

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango akizindua pikipiki 300 kwa ajili ya kazi za maofisa ugani. Ilikuwa Januari 17, 2022

# Serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia ilivyogusa kila eneo la sekta ya mifugo

Na MWANDISHI WETU

NI mwaka mmoja sasa tangu Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, iingie madarakani. Katika kipindi hiki cha uongozi wa serikali ya awamu ya sita shughuli mbalimbali za maendeleo zimeendelea kutekelezwa katika sekta mbalimbali ili kuwaletea maendeleo wananchi wake, mojawapo mwa sekta zinazoendelea kupewa msukumo mkubwa ni sekta ya mifugo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki anaanika mafanikio hayo akisema serikali imeendelea kutekeleza kazi mbalimbali kwa lengo la kuleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Ndaki anasema mafanikio mengi yamepatikana katika Serikali ya Awamu ya sita kupitia sekta ya mifugo,moja ya mafanikio hayo ni udhibiti wa magonjwa ya mifugo na upatikanaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo.

Kwa mujibu wa Waziri Ndaki, Serikali imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuzalisha chanjo ya magonjwa ya kipaumbele ambapo dozi 128,146,275 zimezalishwa kupitia taasisi ya chanjo (TVI) pamoja na Sekta Binafsi. Sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuimarisha taasisi ya chanjo kwa kupatia mashine na vifaa vya thamani ya shilingi 2,400,000,000 huku Kampuni binafsi ya NOVABI ikizalisha dozi 50,000,000 za chanjo tatu, moja dhidi ya ugonjwa wa mdondo, ndui ya kuku na mafua ya kuku.

"Uwekezaji wa sekta binafsi pia umesaidia ongezeko la uzalishaji wa chanjo hapa nchini ambapo Kampuni ya Hester Bioscience Africa Limited katika kipindi hiki cha mwaka mmoja imezalisha dozi 6,130,000 dhidi ya magonjwa ya CBPP, PPR, Mdondo na Gumboro na dozi 609,274,706 za chanjo zimetolewa dhidi ya magonjwa ya mifugo, "anafafanua.

Aidha, Waziri Ndaki anasema, "Kufuatia uchanjaji, milipuko ya magonjwa imepungua hususan Kimeta toka milipuko mitano (5) kwa mwaka, mpaka miwili (2) huku milipuko ya magonjwa mengine nayo ikipungua, mfano mdondo, kichaa cha mbwa, sotoka ya mbuzi, homa ya mapafu ya ng'ombe na homa ya mapafu ya mbuzi.

Kuhusu udhibiti wa magonjwa kwa njia ya uogeshaji, Serikali imenunua lita 33,759 za dawa za kuogesha mifugo kwa shilingi 1,390,000,000 na kuwezesha wastani wa michovyo 462,167,216 kwa ng'ombe 289,097,367, mbuzi 198,958,720 na kondoo 111,943,913 na kusaidia kupunguza matukio ya magonjwa yaenezwayo na kupe kwa asilimia 31.8."

Katika hatua nyingine, anasema Serikali imeimarisha udhibiti wa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine kwa kuwezesha ujenzi wa majosho mapya 230 na ukarabati wa majosho 80 kwa shilingi 3,949,213,000.

Waziri Ndaki anaongeza, "Aidha, katika kuhakikisha shughuli za sekta ya mifugo zinaenda vyema Serikali imeboresha shughuli za ugani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kununua pikipiki 300 na kugawa katika halmashauri hizo huku ikijenga na kukarabati minada 11 kwa shilingi 7,783,004,976 ili kuwezesha biashara ya mifugo.

Biashara ya nyama imeendelea kuimarika ambapo tani 1,774.29 za nyama zenye thamani ya shilingi bilioni 9.91 ziliuzwa nje, na kuanzia mwezi Julai, 2021 mpaka Januari, 2022 jumla ya tani 9,668 za nyama tayari zimeshauzwa nje ya nchi."

Kuhusu ngozi, anasema Tasnia ya Ngozi imeendelea kuimarisha sekta binafsi na kuwezesha uzalishaji wa viatu vya ngozi jozi 3,004,700 huku jumla ya vipande vya ngozi 73,607 vyenye thamani ya shilingi 460,043,750 viliuzwa nje ya nchi.

Katika kuimarisha Tasnia ya Maziwa hapa nchini, Waziri Ndaki anasema Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imewezesha uwepo wa vituo 238 vya kukusanya na kupooza maziwa, viwanda vya kusindika maziwa 104 na kufanya uzalishaji wa maziwa kuongezeka kwa asilimia 12.1 kutoka lita bilioni 2.7 hadi kufikia lita bilioni 3.1.

"Aidha, Serikali imeanza kufanya utambuzi wa mifugo kwa mfumo wa kielektroniki na mpaka kufikia Januari, 2022 jumla ya mifugo 1,504,659 katika mikoa 14 imewekewa hereni za kielektroniki na kusajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi kwa mchanganuo wa ng'ombe 1,219,481, mbuzi 167,298, kondoo 61,571 na punda 56,309.

Kwa upande wa Rasilimali za Maji na Malisho kwa Mifugo, Serikali imechimbaji visima viwili (2) virefu na kukarabati malambo matatu (3) katika katika Halmashauri nne (4) huku ikiwezesha kupima na kutenga jumla ya Hekta 222,525.76 kwa ajili ya malisho ya mifugo katika Halmashauri nne (4) na kufanya eneo la malisho lililotengwa kufikia hekta 3,011,426.92," anaongeza Waziri Ndaki.

Aidha, Serikali imeanza kufanya utambuzi wa mifugo kwa mfumo wa kielektroniki na mpaka kufikia Januari, 2022 jumla ya mifugo 1,504,659 katika mikoa 14 imewekewa hereni za kielektroniki na kusajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi kwa mchanganuo wa ng'ombe 1,219,481, mbuzi 167,298, kondoo 61,571 na punda 56,309.



Uhamasishaji wa hereni za kielektroniki kwa mifugo

# Ripoti samaki kufa Mto Mara yatolewa

Na Richard Mahere, MWANZA

SIKU nne baada ya samaki aina ya sato kuonekana wakielea wakiwa wamekufa ndani ya Mto Mara mkoani Mara, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria imetoa matokeo ya utafiti wa sampuli za maji walizopima katika maabara yao.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha samaki hao wamekufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni kutokana na kuwapo mafuta aina ya oili na grisi yaliyotanda juu ya maji eneo la Mto Kirumi.

Mwanzoni mwa mwezi huu, samaki walionekana wakielea huku wakiwa wamekufa katika mto huo na kuzua taharuki kwa watu wanaopakana na eneo hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Mwanza, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu, alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwapo kiwango kikubwa cha mafuta aina ya oili na grisi.

Alisema katika maji hayo wamebaini kuwapo kiwango kikubwa cha mafuta hayo kuliko kinachokubalika kwa mujibu wa viwango vya ubora wa maji Tanzania cha TZs 2068 2017.

Shinhu alisema kukosekana kwa hewa ya oksijeni ndani ya maji kumesababisha vifo vya viumbe hai wakiwamo samaki.

Kuhusu maji kuwa meusi na kutoa harufu mbaya, mkurugenzi huyo alisema wanaendelea na uchunguzi ili kubaini hali hiyo imetokana na nini.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo hakusema yalikotoka mafuta hayo yaliyotanda juu ya maji kwenye mto huo, zaidi ya kubainisha kuwa chini ya Daraja la Kirumi kumetanda mafuta hayo, akisisitiza bado wanaendelea na uchunguzi.

Habari kutoka katika vijiji vinavyopakana na mto huo, zinadai wananchi ambao wanatumia maji hayo kwa ajili ya kunywa, kunywesha mifugo na kufanya shughuli za uvuvi, wameingiwa hofu.

Licha ya samaki hao kufa wenyewe, baadhi ya wananchi wametumia fursa hiyo na kuingia mtoni na kuwaokota kisha kuwauza kwa wananchi kwa bei rahisi.

Vijiji vilivyokumbwa na tatizo hilo ni pamoja na Kuruya, Kwibuse na Marasibora na maji hayo yaliyochafuliwa yanaingia katika Ziwa Victoria, jambo ambalo linaweza kusababisha samaki zaidi kufa ziwani.

Akizungumzia sakata hilo siku nne zilizopita, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamutamu, alisema uchunguzi wa vifo hivyo vya samaki umeanza.

Alisema sampuli za samaki hao zimepelekwa katika maabara ya usalama wa chakula mjini Musoma mkoani Mara ili kujua chanzo cha vifo hivyo.

Scanned with CamScanner



MWANANCHI UK 24

# *Serikali yajipanga malisho ya mifugo*



**'Kwa sasa tuna mifugo milioni 67 inayojumuisha ng'ombe, kondoo, mbuzi na punda, idadi hii kubwa kuliko idadi ya watu. Jancao itsaidia kufuga kisasa.'**
**Ndaki.**

**Ephrahim Bahemu,** Mwananchi

**Dar es Salaam.** Ili kukabiliana na upungufu wa malisho ya mifugo, Serikali inatarajia kuanzisha mashamba 10 ya nyasi aina ya juncao katika kila wilaya nchini na baadaye kusambaza mbegu zake kwa wafugaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amebainisha hilo kwenye warsha ya wadau wa kilimo waliojadili teknolojia hiyo mpya inayotajwa kuwapa suluhisho wafugaji wa nchini China.

"Tunataka kuziba pengo la malisho nchini, ndiyo maana tunaangazia teknolojia hii ili kuleta tija zaidi. Juncao yatasaidia yanapotekea mabadiliko ya hali ya hewa kama ukame na kusababisha kukosekana malisho," alisema.

Ndaki alisema Serikali imeomba fedha kutoka Shirika la Maendeleo la China (China Aid) ili kutekeleza mpango huo.

"Kwa sasa tuna mifugo milioni 67 inayojumuisha ng'ombe, kondoo, mbuzi na punda, idadi hii ni kubwa kuliko idadi ya watu na tunahitaji kuwa na ufugaji ambao mtu anaweza kufuga mifugo mingi katika eneo dogo, jancao itatusaidia," alisema Ndaki.

Scanned with CamScanner